


# UQAB
Jarida la

*Toleo 25 - Jamad-ul-ula 1440 H / Februari 2019 Miladi*


**Marekani Kujitoa Kijeshi Syria**

**Shambulizi La Riverside**

**Hakuna Jipya Katika Sera Mpya ya Marekani Kuhusiana na Afrika!**

**Ndoto ya Marekani**

**Njia ya Mtume (saw) Kuleta Mageuzi - Halaqa 20**

**SWALI/JAWABU: Makubaliano ya Sweden na Athari Yake Juu ya Janga la Yemen**




## Kuzidi kwa Gharama za Maisha
## Uislamu Ndio Tiba

بسم الله الرحمن الرحيم

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Kenya**

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

KUMB: 03/1440 Ijumamosi, 06th Jumada I 1440 H 12/01/2019 M

# Hizb ut Tahrir /Kenya Uzinduzi Rasmi wa Kampeni Maalumu chini ya mwito:
# Kuzidi Kwa Gahrama za Maisha: Uislamu Ndio Tiba

**Taarifa kwa Vyombo vya Habari**

Hizb ut Tahrir /Kenya inafuraha kuzindua rasmi kampeni maalumu itakayoendelea kwa miezi mitatu kwa mwito “Kuzidi kwa Gharama za Maisha: Uislamu Ndio Tiba” itakayoanza Jumapili, 13 Januari 2019 na kuisha mnamo Ijumaa, 5 Aprili 2019.

Lengo la kampeni ni kufichua dori ya ukoloni urasilimali katika kuendeleza matatizo ya kiuchumi kwa ujumla ambayo yanaendelea kulisakama taifa la Kenya ikijumuisha madeni makubwa kufikia Trilioni Ksh.5.7 na raia wakiendelea kuishi maisha magumu na duni. Kampeni hii pia inatarajia kuwasilisha suluhisho la Kiislamu katika kutatua changamoto za kiuchumi kama mfumo kamili ulio na sheria za kutatua matatizo yote yanayowakumba wanadamu.

Ili kufaulisha Kampeni hii, Hizb ut Tahrir /Kenya itaandaa msururu wa matukio ikijumuisha darasa/mihadhara, ziara kwa wasomi wakijumuisha wakiuchumi ndani ya taifa hili pamoja na amali nyinginezo.

Kampeni hii ni moja ya kazi za Hizb ut Tahrir katika kujenga rai jumla kwa kuwasilisha mtizamo safi wa kiuchumi kwa msingi wa Uislamu ambao ulitekelezwa kwa karne 13 na Dola ya Kiislamu ya Khilafah na kutatua kivitendo matatizo ya kiuchumi. Tunaamini kuwa kuvunjwa kwa Khilafah kutokana na mikono ya wamagharibi mwaka 1342H sawia na 1924M ndiyo chanzo cha changamoto za kiuchumi na matatizo jumla yanayoukumba ulimwengu leo. Pia, tuna yakini kuwa suluhisho la kuzidi kwa gharama za maisha na maovu yanayo waandama wanadamu ni kwa kuondosha mfumo wa dhuluma wa kirasilimali na kuweka mahala pake mfumo wa Kiislamu chini ya kivuli cha Khilafah kwa njia ya Mtume Muhammad (saw). Kurudi tena kwa Maisha ya Kiislamu kupitia kusimamisha tena Khilafah ndio itawakomboa tena wanadamu kutoka katika majanga ya kiuchumi na maovu ya kila aina kwa kuutekeleza kikamilifu mfumo wa Uislamu na nidhamu zake ikijumuisha ile ya nidhamu ya kiuchumi wa Uislamu pamoja na sera yake bora iliyomo ndani yake.

Kwa kutamatisha, tunatoa mwito kwa Ummah jumla hususan Ummah wa Waislamu washiriki nasi katika kampeni hii adhimu ambayo inatarajia kuzindusha mengi na ambayo yatatufaa hapa Duniani na Akhera.

**Fuatilia Hashtags Zifuatazo:**
**Kiengereza: #IncreasedCostOfLiving_IslamIsTheSolution**
**Kiswahili: #KuzidiKwaGharamaZaMaisha_UislamuNdioTiba**

**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari wa Hizb ut Tahrir Kenya**

# Kuzidi Kwa Gahrama za Maisha: Uislamu Ndio Tiba
## Sehemu ya Kwanza: Hali ya Kiuchumi ya Kenya

Kenya ilipopata "Uhuru Bandia" mwaka 1963 Pato la Taifa (GDP) lilikuwa Dola za Marekani milioni 926.6 ikiwa na idadi ya watu milioni 8.9 ikiwa ni mgao wa Dola za Marekani 104 kwa kila mtu kwa mwaka. Kufikia mwaka 2018 Pato la Taifa lilikuwa ni Dola za Marekani bilioni 85.98 ikiwa na idadi ya watu takribani zaidi ya milioni 48 ikiwa ni mgao wa Dola za Marekani 1,790 kwa kila mtu kwa mwaka. Takwimu zinaonyesha sekta zinazochangia katika ukuaji wa GDP ni sekta ya huduma (biashara za jumla na rejareja, uchukuzi, fedha n.k), sekta ya viwanda na utengenezaji na sekta ya kilimo mtawalia. Kiasi kufikia Jumanne, 30 Septemba 2014, Kenya ilitangazwa kuwa nchi ya 9 Afrika yenye uchumi mkubwa na kupanda daraja na kuwa "Nchi ya Mapato ya Kati" (https://www.brookings.edu, Ijumaa, 3 Oktoba 2014)

Kwa upande mwengine madeni jumla (nje na ndani) yakadiriwa kufika kiwango cha zaidi ya trilioni Ksh7 mwaka 2020. (The East African, 18 Disemba 2018). Huku Bajeti ya trilioni Ksh3 ya mwaka 2018/2019 ilikuwa na pengo la bilioni Ksh500! Ukuaji wa GDP unaashiria kuwa Taifa la Kenya lipo katika njia imara na wakati huo huo kuzidi kwa madeni kuna ashiria kuwa Taifa liko katika mkondo mbaya mno na unaweza kuipelekea nchi hii kusakamwa na madeni kiasi kwamba uchumi wake utasambaratika.

La kushangaza ni kuwa tangu tupate "Uhuru Bandia" pengo kati ya masikini na matajiri linazidi kukuwa tena kwa kasi kubwa. Licha ya uchumi wa Kenya kuwa mkubwa ndani ya eneo la Afrika Mashariki na Kati na Nairobi kuwa ndio kitovu cha biashara za eneo hilo. Raia nchini Kenya wanazama ndani ya Umasikini kwa asilimia 45.9 (https://www.bbc.com, 30 Septemba, 2014). Kwa maana nyingine zaidi ya Wakenya 4 kati ya 10 wanatumia takribani Dola za Marekani 1.90 kukidhi mahitaji yao!

Kenya ni dola kibaraka wa mkoloni Muingereza; kwa hiyo nidhamu yake ya uchumi inatokamana na mfumo wa kisekula wa kirasilimali ambao imeurithi kutoka kwa bwana wao Muingereza. Kwa hivyo daima haitarajiwi kukuwa kwa uchumi kutapelekea kuboresha hali za raia jumla isipokuwa kwa wachache walio katika mduara maalumu ndani ya utawala na wengine wanabakia pembezoni tu! Sera ya nidhamu ya uchumi wa kirasilimali imekitwa katika kulimbikizia matajiri utajiri na kuwalimbikizia umasikini walala hoi! Lakini kwa sharti kwamba walala hoi waendelee kupawa pumzi wasife ili waendelee kuwatumikia matajiri majumbani na viwandani mwao na vijipesa wanavyopewa kupitia mkono wa kulia kama mshahara vinaporwa tena kupitia mkono wa kushoto kwa njia ya ushuru!

Hali hii itaendelea mpaka pale Wanadamu watakapozinduka na kufahamu kuwa tatizo sio uchumi kukuwa polepole au haraka bali ni itikadi ya kisekula ya kutenganisha dini na maisha ndiyo chanzo cha mashaka tuliyonayo ikiwemo asilimia kubwa ya umasikini wa kupindukia! Itikadi hii na mfumo wake wa kirasilimali zimempa mwanadamu majukumu ya kujipangia namna ya kuishi apendavyo ikiwemo kujitungia sheria mwenyewe namna ya kuendesha mambo yake. Nidhamu zake ikiwemo ya kiuchumi inaendeshwa kwa matamanio ya nafsi za watu, kiasi kwamba badala ya serikali kuendea mbio raia wake wapate mahitaji msingi mfano chakula, mavazi na makaazi wao wanakwenda mbio eti "kuwekeza katika miundo mbinu n.k" ili kuukuza uchumi! Ni uchumi gani ambao unalengwa kukuzwa ilhali madeni yanazidi kuwa makubwa na raia takribani asilimia 50 wanashindwa kukidhi mahitaji yao msingi?!

**Ali Nassoro Ali**
**Mwanachama wa Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Kenya**

## Sehemu ya Pili: Nidhamu ya Uchumi ya Kiislamu chini ya Serikali ya Kiislamu ya Khilafah

Serikali ya Kiislamu ya Khilafah husimama kwa misingi ya sheria za Mwenyezi Mungu (swt) yaani kutoka kwa Shari'ah (Qur'an na Sunnah). Serikali hii ipo kwa ajili ya majukumu mawili msingi nayo ni kutekeleza/kutabikisha Shari'ah ndani ya eneo inalotawala na kueneza Da'wah ya Uislamu ulimwenguni kote ili kuwakomboa kutoka katika utumwa wa kumuabudu mwanadamu hadi kumuabudu Muumba wa viumbe vyote chini ya mfumo wenye uadilifu wa Uislamu.

Miongoni mwa nidhamu za Uislamu ni ile ya Kiuchumi. Nidhamu ya kiuchumi humaanisha utaratibu wa mahusiano kati ya watu na mahitaji yao , njia ya kukimu mahitaji hayo pamoja na ufuatiliaji wa njia za kufikia kukidhi mahitaji hayo. Uislamu unatambua kuwa mwanadamu ni mwenye kikomo na hivyo basi mahitaji yake yana kikomo na kuyafunga katika viungo vyake na ghariza zake. Njia (mali) za kushibisha ziko nyingi na zimetapakaa dunia nzima. Ufuatiliaji (usambazaji) wa njia hizo ndio chanzo cha matatizo ya kiuchumi yanayomkumba mwanadamu kutokana na suala la umiliki. Ili tuweze kuyatatua, ni lazima tuirudie fikra inayotokamana na itikadi (mtizamo juu ya maisha). Itikadi ya Uislamu ni Hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa Haki isipokuwa Mwenyezi Mungu na Muhammad ni Mtume wake. Kwa msingi huo nidhamu ya kiuchumi wa Kiislamu imekuja kutatua tatizo la usambazaji wa mali kwa mujibu wa Shari'ah. Kinyume chake ni kuwa itikadi ya Kisekula inayotenganisha dini na maisha; inasema kuwa tatizo la kiuchumi linalomkumba mwanadamu ni uhaba wa bidhaa na huduma haziwezi kukidhi mahitaji mengi ya mwanadamu! Na suluhisho lao la kiuchumi ni warasilimali (wenye viwanda) kuendelea kuzalisha bidhaa na huduma ili ziweze kukidhi mahitaji ya wanadamu!

Sera ya Uchumi wa Kiislamu chini ya Khilafah ipo

*Endelea Uk..4*

kuhakikisha kuwa kila binadamu (raia wake) anaweza kukidhi mahitaji yake msingi kwa ukamilifu nayo ni chakula, mavazi na makaazi na kumuewezesha kukidhi mahitaji ya ziada. Mtu anaweza kukidhi mahitaji yake kupitia kufanya kazi. Na ikiwa hawezi kufanya kazi atasimamiwa na msimamizi wake, ikiwa msimamizi wake hawezi; Serikali itamsimamia. Ndani ya Khilafah hakuna utozwaji ushuru/ kodi kama inavyoshuhudiwa leo mfano (PAYE, VAT, NHIF, NSSF, Housing Fund n.k). Na hii ina maana Uislamu tayari umedokeza njia za kukusanya mapato yake na jinsi ya usambazaji au matumizi yake. Mapato haya ni kama vile Zaka, Kharaj na Ushru Fai n.k. Ama suala la kutoza ushuru kama ilivyo leo katika mataifa ya kibepari kama Kenya, hakika halipo katika Uislamu ila kwa dharura maalum nayo ikiondoka utozwaji ushuru ni haramu. Hali hii inapelekea maisha kuwa mepesi kwani watu wataweza kumudu bei ya huduma na bidhaa kinyume na ilivyo sasa chini ya dola za kisekula ikiwemo Kenya!

Uislamu umegawanya mali makundi matatu mali; ya mtu binafsi, mali ya ummah na mali ya serikali ya Khilafah. Mali ya mtu binafsi ni anayomiliki na kuitumia kwa njia ya Halali pekee. Mtu binafsi anaweza kupata mali kupitia njia tano: kufanya kazi, kurithi, kupokea matumizi ya kukidhi mahitaji, ruzuku ya Serikali kwa raia wake na Mali anayopata mtu pasi na kutumia fedha au kufanya kazi (kupewa zawadi n.k). Mali ya Ummah ni vitu ambavyo Muumba amevifanya umilikaji wake ni wa Waislamu wote. Na kuwaunganisha katika umilikaji na kuzuia watu binafsi kumiliki mfano vizalishavyo umeme, kawi, viwanda vya gesi, makaa na madini ambayo yako kwa wingi na hayaishi ima yaliyo imara kama dhahabu, chuma au majimaji kama mafuta, gesi mfano gesi ya kawaida, bahari, maziwa, misitu, misikiti vyote hivyo na mfano wake ni Mali ya Ummah inamilikiwa na Waislamu wote, umiliki wa pamoja na ni mapato ya Bait ul Mal ya Waislamu,wakiganyiwa na Khalifah kwa mujibu wa Shari'ah. Mali hii Khalifah haruhusiwi kumpa umilikaji mtu yeyote ima mtu binafsi au kikundi maanake ni ya Waislamu wote kwa pamoja.

الْمُسْلِمُونَ شُرَكَاءُ فِى ثَلاَثٍ الْمَاءِ وَالْكَلإِ وَالنَّارِ
Waislamu ni washirika katika matatu: maji, malisho, moto
[Ahmad na Ibn Maja]

Mali ya Serikali ya Khilafah ni chochote katika ardhi au jengo linalohusiana na haki ya Waislamu wote; inatenganishwa na Mali ya Ummah. Mali ya Serikali inaweza kuwa ardhi, majengo, vitu vya kuhamishika ambavyo vimefungamanishwa na haki ya Waislamu jumla kwa mujibu wa Shari'ah. Khalifah ana mamlaka ya kusimamia, kuichunga na kufanya maamuzi kuhusiana na mali hiyo. Mali hii Khalifah anaruhusiwa kupeana umiliki wake mtu yeyote, kupeana hatimiliki na manufaa au manufaa bila umiliki au kuruhusu waziboreshe na wazimiliki, na anaweza kuitumia katika njia anayoona ni kwa maslahi ya Waislamu. Khalifah ameruhusiwa kupeana umilikaji wa ardhi kwa ambaye hana ardhi ya ukulima, mtu huyo ailime na iwe mali yake.

كَىۡ لَا يَكُونَ دُولَةَۢ بَيۡنَ ٱلۡأَغۡنِيَآءِ مِنكُمۡۚ
ili yasiwe yakizunguka baina ya matajiri tu miongoni mwenu.
[Al-Hashr: 7]

Khalifa hana ruhusa ya kuchukua mali ya mtu binafsi na kisha kumpa mtu mwengine, lakini anweza kupeana kutoka katika Mali ya Serikali na kuwapa masikini na sio matajiri. Mali hizi zimewekwa na Shari'ah hairuhusiwi kubadilisha mpangilio wake, kiasi kwamba Mali ya Ummah kubadilishwa na kuwa Mali ya Mtu Binafsi. Mfano kupeana haki za kutafuta na kuchimba mafuta kwa kampuni binafsi inayoitwa "ubinafsishaji" huku ni kuibadilisha Mali ya Ummah na kuifanya kuwa ya Mtu Binafsi. Vivyo hivyo hairuhusiwi kuhamisha umiliki wa Mali ya Mtu Binafsi na kuifanya kuwa Mali ya Serikali. Mfano kutumia nguvu kuchukua duka la mtu na kulifanya la Serikali inayoitwa "utaifishaji"

Uislamu chini ya kivuli cha Khilafah utahakikisha raia wamo ndani ya mazingira ya uchajimungu na kuwapelekea kuhurumiana baina yao: Waumini katika kuhurumiana kwao ni kama mwili mmoja. Wakati kiungo kimoja kinaumwa, mwili mzima unashughulishwa kwa kuupelekea kuwa na homa na kukosa usingizi.
[Bukhari na Muslim]
Kuhurumiana huko ni kwa raia jumla chini ya Khilafah kutokana na utekelezaji wa Shari'ah ambao unajumuisha uhalalishaji wa biashara na uharamishaji wa riba, michezo ya bahati nasibu, udanganyifu katika biashara, ukiritimba wa mali na biashara, kufunga bei juu ya bidhaa au huduma n.k. Kutokana na utelekezwaji wa Uislamu kwa ukamilifu wake ndani ya Karne Kumi na Tatu hadi kuangushwa kwake 28 Rajab 1342 Hijria sawia na 3 Machi 1924 Miladi raia chini ya Khilafah waliweza kuona kivitendo namna nidhamu ya kiuchumi ya Uislamu ilivyo wanyanyua binadamu kutoka katika umasikini. Hali hiyo itarudi tena punde tu maisha ya Kiislamu yakataporudi kupitia kusimamishwa kwa Serikali ya Khilafah kwa njia ya Utume.

Kinyume chake ni kuendelea kutaabika ndani ya dola hizi za kisekula za kikoloni. Daima zinawakandamiza raia wake kiuchumi kupitia ushuru na kodi ambazo kiasili zisingestahili kutozwa raia. Huku zikishirikiana na taasisi za kikoloni kama Benki ya Dunia na Taasisi ya Fedha ya Kimataifa, na kuchukua mikopo ya mataifa kama China, Uingereza n.k kuwafunga katika minyororo ya madeni yaliyo na riba! Mali zote ambazo Kenya imeruzukiwa na Mwenyezi Mungu ikiwemo madini, mafuta, ardhi za ukulima n.k; zote zimebinafsishwa na kumilikiwa na watu binafsi ilhali raia jumla wamebakia kudidimia katika umasikini wa kupindukia! Waliobahatika kuajiriwa hulipwa mishahara duni kwa kutegemea makadirio ya matumizi yake kwa kiwango cha chini na kisha kiwango hicho hicho kinatozwa ushuru na kodi zisizoingia akilini! Serikali hizi daima ziko mbioni kupigia debe eti "kulipa ushuru ni kujitegemea!" Na kujitia upofu wakati makampuni ya kikoloni yanaendeleza uporaji wa mali za Ummah na kuyafanyia wepesi katika "uwekezaji wao" kwa kuyaondolea ushuru na kodi!

**Ali Nassoro Ali**
**Mwanachama wa Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Kenya**

# Habari & Maoni
## Marekani Kujitoa Kijeshi Syria; Kuna nini nyuma yake?



**Habari:**

Trump Aondosha Majeshi ya Marekani kutoka Syria.

**Maoni:**

Tangazo la Trump kuondosha jeshi ndani ya Syria limezua patashika ya upinzani ndani ya bunge la Congress, na hata kutoka kwa watu muhimu ndani ya Chama cha Republican. Pia, Kamanda wa Marekani wa Afisi Kuu ya Majeshi, Jenerali.Joseph Votel na balozi wa Marekani wa muungano wa wanaopigana na Islamic State, Brett H. McGurk, walipinga vikali kuondoshwa kwa jeshi, ikisababisha kujiuzulu kwa Waziri wa Usalama Jim Mattis. Lakini wa mwanzo kabisa kuonesha wasiwasi mkubwa walikuwa ni wa Kurdi kutoka Syria.

Kwa hiyo maswali yanajitokeza, ni kwa nini Trump amekakamia maamuzi yake licha ya upinzani wote huu? Je ni kitendo cha kukurupuka cha Trump au ni sehemu ya mpango mpana?

Kwanza, ni lazima ieleweke kuwa kujitoa kwa jeshi haimaanishi kwa hali yoyote ile kuwa inaashiria kujitoa kwa Marekani au athari yake juu ya eneo. Na hususan lau jeshi litatoka itajumuisha tu sehemu ndogo ambayo haizidi elfu kadhaa ya wanajeshi kwa mujibu wa hali ya Syria. Lakini historia inatufunza kinyume chake. Uvamizi wa kijeshi wa kigeni au uwepo wa jeshi ni moja ya ala nyingi za dola za kikoloni katika kufikia malengo yao.

Hili lilisemwa wakati wa nyuma Machi 2018, Trump alisema kuwa atawaregesha wanajeshi nyumbani punde "watakaposhinda vita." Hakuweka siku maaalumu lakini alieleza malengo yake wakati huo pasi na upinzani wowote. Lakini hivi sasa yuko tayari kulitekeleza hili, kelele zinachipuza kama ambaye halikukuwepo suala hili. Kwa hiyo, upinzani dhidi ya maamuzi ya Trump lazima yatathminiwe kwa mtizamo kwamba tayari kuna mzozo baina ya baadhi ya pande husika ndani ya Marekani na Trump.

Licha ya tofauti hizi ambazo zimetokamana na njia na rasilimali, mpango wa Marekani juu ya Syria ulikuwepo wazi. Utawala wa Syria na nidhamu yake ya kisekula lazima ubakie ima Bashar al-Assad awepo au asiwepo, na upinzani ulio na mradi wa Kiislamu lazima upunguzwe kasi, udhibitiwe na umalizwe. Hili linafupisha kwa uhakika sera ya Marekani ndani ya miaka 7 iliyopita ndani ya Syria pamoja na washirika wake, Uturuki, Iran na Urusi.

Kutokana na sera hii, Utawala dhaifu wa Syria uliweza kudhibiti tena takribani kila eneo ndani ya Syria isipokuwa eneo la Idlib ambapo kumebakia chembechembe za upinzani hivi sasa na eneo la Kaskazini ambapo wa Kurdi wanamiliki eneo lao wanalojitawala. Mchezo unakaribia kuisha. Kikwazo pekee dhidi ya kuunganisha na kuufufua tena utawala wa Syria ni upinzani wa Syria na wa Kurdi walioko Kaskazini.

Ama kuhusu eneo la Kikurdi, Marekani imewajenga na kuwalinda dhidi ya Uturuki na imewatumia kikamilifu

*Endelea Uk..6*

katika kupigana na kundi la Bagdadi na makundi ya Kiislamu. Marekani kujitoa kijeshi kutawaacha wakiwa hawana mtetezi dhidi ya tishio la Uturuki na upande mwingine tishio la Bashar al-Assad ambaye anataka kuiweka Syria yote chini ya udhibiti wa serikali yake.

Ndio sababu viongozi wa Kurdi walihisi joto na haraka wakazindua mazungumzo ya pande mbili na Damascus kuhusu makubaliano ya makaazi waliposikia kuhusu kujitoa kwa Marekani. Kwa hiyo wa Kurdi wamelazamishwa kiujanja kufanya mazungumzo na utawala wa Syria ambayo hatima yake ni kuunganishwa kwa Kaskazini ya Syria kuwa Syria "iliyoungana."

Pia, majibu muhimu lakini ya kujieleza yalitoka kwa Waziri wa Kigeni wa Uturuki Mevlut Cavusoglu. Alisema kuwa Uturuki na viongozi wa kiulimwengu watashauriana kuhusu kufanya kazi na Rais wa Syria Bashar al-Assad lau atashinda kura za kidemokrasia. Na Rais wa Sudan Omar al-Bashir akamzuru Bashar al-Assad na kumfikishia matumaini yake kuwa Syria hivi karibuni itarudi tena katika dori yake muhimu ya kieneo. Kwa kuitambua rasmi serikali hii ya kimauaji, inafichua na wakati huo huo inadhibitisha mpango unaofuata wa Marekani.

Mazungumzo kuhusu kurudi kwa Syria katika Muungano wa (Arab League) tayari yanaendelea. Hili lilielezewa na mtu katika makao makuu ya Muungano huo mjini Cairo siku ya Alhamisi pamoja na Sputnik.

Mapema, chanzo katika serikali ya rais wa Tunisia kilisema kuwa nchi nyingi za Kiarabu ikijumuisha Tunisia na Algeria, zinashirikiana katika juhudi za kuirudisha Syria katika shirika hilo. Kwa mujibu wa mzungumzaji, Tunisia, Iraq na Algeria ziko mbioni kuhakikisha kuwa Syria inashiriki tena katika kazi za Muungano huo.

Kujitoa kwa Marekani kulipongezwa na Wizara ya Kigeni ya Urusi kwa kusema kuwa hatua hiyo itatoa nafasi ya mchakato wa kisiasa ndani ya Syria.

Na mazungumzo ya pande mbili kati ya Trump na Erdogan kabla ya kutangaza kujitoa, kunadhibitisha kuwa kujitoa kwa Marekani sio kitendo cha kukurupuka bali ni mpango ndani ya mpango mpana muovu wa kuyamaliza mapinduzi ndani ya Syria pamoja na washirika wake.

وَإِذْ يَمْكُرُ بِكَ الَّذِينَ كَفَرُوا لِيُثْبِتُوكَ أَوْ يَقْتُلُوكَ أَوْ يُخْرِجُوكَ وَيَمْكُرُونَ وَيَمْكُرُ اللَّهُ وَاللَّهُ خَيْرُ الْمَاكِرِينَ

"Na [kumbuka, Ewe Muhammad], walipo kupangia mpango walio kufuru wakufunge, au wakuuwe, au wakutoe [kutoka Makkah]. Wakapanga mipango yao, na Mwenyezi Mungu akapanga yake. Na Mwenyezi Mungu ndiye mbora wa mipango. [Al-Anfal: 30]

**Okay Pala**
**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari wa Hizb ut Tahrir Netherlands**

بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Kenya**

﴿وَعَدَ ٱللَّهُ ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ مِنكُمۡ وَعَمِلُواْ ٱلصَّٰلِحَٰتِ لَيَسۡتَخۡلِفَنَّهُمۡ فِي ٱلۡأَرۡضِ كَمَا ٱسۡتَخۡلَفَ
ٱلَّذِينَ مِن قَبۡلِهِمۡ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمۡ دِينَهُمُ ٱلَّذِي ٱرۡتَضَىٰ لَهُمۡ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّنۢ بَعۡدِ خَوۡفِهِمۡ أَمۡنٗاۚ
يَعۡبُدُونَنِي لَا يُشۡرِكُونَ بِي شَيۡـٔٗاۚ وَمَن كَفَرَ بَعۡدَ ذَٰلِكَ فَأُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلۡفَٰسِقُونَ﴾

حزب التحرير
HIZB UT TAHRIR

KUMB: 04/1440 Alhamisi, 11 Jumada I 1440H 17/01/2019 M


# Shambulizi La Riverside Lisitumike Kuendeleza Vita Dhidi ya Uislamu

**Taarifa kwa Vyombo vya Habari**

Hizb ut Tahrir /Kenya imeshtushwa na mauaji ya watu 14 yaliyotokea katika hoteli ya Dusitd2 iliyoko eneo la Riverside, Nairobi. Sisi Hizb ut Tahrir /Kenya tunapinga vikali umwagaji damu na wakati huo huo tunasema yafuatayo:

Kwa kuwa kuna ripoti kuwa wahusika katika shambulizi hili wameuawa, tunatoa mwito kwa vyombo vya usalama nchini Kenya visiwasumbue raia wasiokuwa na hatia. Lakusikitisha imekuwa jambo la kawaida kwa polisi kuiandama jamii ya Waislamu kwa kisingizio kuwa wanaimarisha usalama.

Shambulizi hili la hoteli limetokea licha ya serikali kudai kuwa imeboresha usalama; hivyo basi, suali msingi ni: *"Waliwezaje washambulizi hao kutumia gari lililokuwa na nambari za usajili za Kenya, kuingia hotelini na kufanya uovu huo?"* Tunasema kwa kinywa kipana kuwa ni jukumu la vyombo vya usalama kuhakikisha usalama kwa raia na mali zao.

Ama kuhusu vyombo vya habari vya humu nchini na vya kimataifa, vilipatiliza na kusema kuwa tukio hili ni kitendo cha ugaidi na kuwalaumu Waislamu na Uislamu kabla hata serikali kutoa kauli yake. Tunakichukulia kitendo chao hicho ni cha kimakusudi na kinalenga kuupaka matope Uislamu na kusababisha chuki za kidini kati ya jamii. Tunasema kwamba tawala za Kimagharibi hupatiliza mashambulizi mfano huu katika kuendeleza upotoshaji juu ya Uislamu kwa kisingizio cha kupambana na ugaidi. Lakuvunja moyo zaidi, ni kwamba Wamagharibi katika kiu chao cha kupora mali za mataifa mengine, wanashirikiana na madikteta kufanya mauaji ya halaiki mfano Syria, Iraq, Sudan Kusini na maeneo mengine. Bila kuona haya, ugaidi wao wanauita ukombozi wa kumakinisha Demokrasia!

Kwa kutamatisha, tunatoa nasaha ya haki kwa Wasomi Waislamu wasiingie katika mtego wa Wamagharibi katika kuukashifu Uislamu kuwa ni chanzo cha ugaidi. Tunawakumbusha kuwa Wamagharibi hawatochoka katika kupambana na Uislamu na Vita dhidi ya Ugaidi vimelengwa kuwalazimisha Waislamu kuachana na mafunzo yao ya Kiislamu. Zaidi ya hayo, tunaamini kuwa wafuasi wa dini zilizopo hawatokubali mafundisho yao kuingiliwa au kubadlisha misimamo yao ya kidini kutokamana na kulazimishwa na wengine. Wamagharibi hawapigani na ugaidi wa kweli, bali wanawataka Waislamu wasijifunge kikamilifu na Uislamu wao kama mfumo bora na wenye uwezo wa kutatua matatizo yanayowakumba wanadamu leo. Hizb ut Tahrir /Kenya inasisitiza kwamba Uislamu tokea mwanzo hadi mwisho wa dunia, unapinga vitendo vyote vya vurugu ima vimefanywa na Waislamu au wasiokuwa Waislamu.


**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari wa Hizb ut Tahrir Kenya**

# Hakuna Jipya Katika Sera Mpya ya Marekani Kuhusiana na Afrika!




Utawala wa Donald Trump ulizindua ile inayoitwa "Sera Mpya ya Afrika" siku ya Alhamisi tarehe 14 Disemba 2018 katika Taasisi ya Heritage huko Washington DC kupitia Mshauri wa Usalama wa Kitaifa, John Bolton. Sera hiyo imekitwa katika misingi ifuatao: 1.Kupanua biashara ya Marekani na mahusiano ya kibiashara kati yake na mataifa ndani ya eneo lote, 2.Kupambana na hofu juu ya Uislamu wenye misimamo mikali na ugaidi na mizozo ya kivita na 3.Kutathmini upya dori ya uenezaji amani Afrika kwa kutosaidia na kutowekeza katika misheni za Umoja wa Mataifa (UN) ambazo hazizalishi, hazifaulu na hazihesabiki.

Kwa mara nyingine sera hii imedhihirisha kuwa Afrika inacheza dori muhimu katika njama za Wamagharibi. Kwani, tokea mwanzo Wamagharibi wanaitizama Afrika kama shamba la kikoloni ambalo lastahili kuporwa na watu wake kufanywa watumwa katika kila nyanja ya maisha ikijumuisha kijamii, kiuchumi, kisiasa na kielimu kwa kuwatekelezea mfumo batili wa kisekula wa kirasilimali na nidhamu zake zinazochipuza kutokana nayo.

Uzinduzi wa sera hiyo unafanyika wakati ambapo Marekani imeanzisha Vita vya Kiuchumi vya Karne ya 21 dhidi ya maadui wake wa kweli na inaowadhania ambao wanaojumuisha Umoja wa Ulaya, China, Urusi na marafiki zao mtawalia. Maslahi ya Marekani yaliyomakinishwa juu ya mwito wa "Make America Great Again" ndiyo inayoendesha vita hivi. Misingi mitatu ya sera hiyo inamulika wazi aina ya mahusiano kati ya Afrika na Amerika, kuwa ni kati ya mtumwa na bwana. Kwa kuwa Afrika ni soko la ununuzi wa bidhaa za magharibi, ambazo mali ghafi yake imetoka katika shamba la kikoloni na hivyo basi biashara yake inaegemea Magharibi kuliko mataifa mengine. Ama kuhusu vita juu ya Uislamu wenye misimamo mikali, ni njama tu ya Wamagharibi ili kuwadanganya watu kuwa kujifunga kikamilifu na Uislamu ni tishio kwa dini nyingine. Lakini, ukweli wa nia yake ya kuushambulia Uislamu na Waislamu chini ya pazia ya kupigana na Uislamu wenye misimamo mikali na ugaidi na mizozo ya kivita; ni kuupaka matope Uislamu kama mfumo badala ya ule batili na uliofeli wa kisekula wa kirasilimali ambao umesababisha majanga kwa binadamu ulimwenguni kote. Ama kuhusu "UN kueneza amani," ni urongo mwingine unaopigiwa debe na utawala wa Marekani ilhali wao ndio waanzilishi wa vita duniani kwa kuzivamia nchi nyingine ima moja kwa moja au kupitia mawakala ili kufikia malengo yake maovu.

Sera hii haina tofauti na zile za Umoja wa Ulaya, China, Urusi na washirika wao mtawalia katika mtizamo wao juu ya Afrika na hususan Waislamu na Uislamu. Ama kuhusu Afrika hili ni jaa lao la kumwaga bidhaa walizotengeneza ambazo chanzo cha mali ghafi yake rahisi imeibiwa moja kwa moja au kudhaminiwa na watawala vibaraka! Ama kuhusu Waislamu na Uislamu, ni tishio kwa utawala ulioko mamlakani ulimwenguni chini ya kivuli cha mfumo wa kisekula wa kirasilimali na nidhamu zake zinazonuka na zilizotokana nao. Na ndiyo maana tunao mfano wa Waislamu wanaoteseka ndani ya jela za Urusi, China, Guantanamo Bay chini ya Marekani na katika nchi zilizoko chini ya Umoja wa Ulaya na koloni zake za awali zinapitishia sheria zisizokuwa na huruma kumpana dhidi ya eti "Ugaidi na Misimamo Mikali." Hatua zote hizi ni

***Endelea Uk..9***

kuhakikisha kuwa Uislamu haurudi tena kama mfumo kamili wa maisha chini ya kivuli cha Khilafah kwa njia ya Utume.

Tunaipinga hii sera mpya ya Afrika ambayo imeboreshwa na Marekani kwani inazindua upya wimbi la kung'ang'ania Afrika dhidi ya mataifa mengine makubwa ambayo yanajitahidi kuipiku Marekani katika kulimiki bara la Afrika. Wakati huo huo tunaulingania uongozi wa Afrika uukumbatie ulinganizi wa Khilafah ili kuweza kufikia mwamko wake na kuweza kukata mahusiano ya waporaji.

**Hizb ut Tahrir Kenya** inawakumbusha viongozi na wanasiasa wa bara la Afrika wawe wakweli kwa watu wao na wayaunge mkono maslahi ya raia wao. Kwa kupitia kukataa siasa za Marekani mkoloni ambazo zimefichua ukoloni mambo leo waziwazi. Hadi lini bara hili ambalo limejaa utajiri wa rasilimali lakini ndilo masikini ulimwenguni litafikia upeo wake? Ni mpaka viongozi ambao wamesalimisha nafsi zao kwa agenda za kikoloni zikiongozwa na Amerika, waachane na kujinasuwa na utumwa wa mfumo muovu kwa kutafuta njia ya maisha badala ambayo itawapa watu hadhi na kuwalinda damu na rasilimali zao. Historia itawahukumu vibaya mno!

**Hizb ut Tahrir Kenya** inawapa changamoto wanafikra na wasomi ambao ni wakweli kwa watu wao waupinge ukoloni wa mambo leo kwa kutumia akili, midomo na maandishi yao. Uzinduzi wa sera hii haumuhitaji msomi kutambua ni muendelezo wa uporaji, unyanyasaji na ubabe dhidi ya bara la Afrika. Mpango wenyewe uko wazi kuwa ni kwa maslahi ya Marekani kiuchumi kisiasa, usalama… chini ya mwito wa "Marekani kwanza" licha ya athari itakayopatikana kwa bara zima la Afrika. Huu ndio uhalisia wa nidhamu ya kikoloni ya kirasilimali, kwani mahusiano kati ya nchi kubwa na ndogo ni mahusiano ya Bwana na mtumwa wake. Hakuna Bara lililoathirika zaidi na nidhamu hii kama Afrika! Haijawalazimu kwenu kutafuta mfumo badala ili kuwaokoa watu ambao wanaokutizameni, basi fahamu zenu zitawaadhibu!

**Hizb ut Tahrir Kenya** inawakumbusha Waislamu dori ya ulinganizi wa Uislamu kama mfumo wa maisha ulio na suluhisho juu ya matatizo ya mwanadamu na kuwahesabu viongozi ambao wanaiga kila kitu kutoka Magharibi kiasi kwamba inapelekea kuharibu nchi zao na watu wao.

"وَ اِذَا قِيۡلَ لَهُمۡ لَا تُفۡسِدُوۡا فِى الۡاَرۡضِۙ قَالُوۡۤا اِنَّمَا نَحۡنُ مُصۡلِحُوۡنَ اَلَاۤ اِنَّهُمۡ هُمُ
الۡمُفۡسِدُوۡنَ وَ لٰـكِنۡ لَّا يَشۡعُرُوۡنَ"

"Na wanapo ambiwa: Msifanye uharibifu ulimwenguni. Husema: Bali sisi ni watengenezaji. Hakika wao ndio waharibifu, lakini hawatambui."﴾Al-Baqara:11-12﴿

**Hizb ut Tahrir Kenya**
**05 Jumadal Awwal 1440 Hijria**
**11/01/2019 Miladi**

# Somalia Iliyomakinika Kisekula: Ndoto ya Marekani

Vyombo vya habari vimeripoti kushikwa kwa Mukhtar Robow "Abu Mansur" siku ya Alhamisi, 13 Disemba 2018 akiwa katika mkutano wa kawaida ulioitishwa na rais mshikilizi wa Jimbo la Kusini Magharibi ya Somalia mjini Baidoa. Alishikwa na maafisa wa Ethiopia na mara moja kuhamishwa kambi ya jeshi ya Ethiopia viungani mwa mji kabla kwenda naye Mogadishu.

Mukhtar Robow "Abu Mansur" alikuwa makamu kiongozi na msemaji wa kundi la Al-Shabaab, ambalo mwanzoni lilibuniwa kupigana na "uvamizi wa Ethiopia." Kabla kujiunga na Al-Shabaab, mwanzoni mwa miaka ya 2000 alishiriki katika Jihad dhidi ya Soviet ndani ya Afghanistan ambayo ilipigiwa debe hususan na Saudi Arabia, Pakistan na Amerika. Kisha alikuwa kiongozi wa muda mrefu wa Vuguvugu la Kiislamu la Somalia, alisaidia kuijenga tena Al Itihaad Al Islamiyya ambayo ilisambaratishwa mnamo 1997 na jeshi la Ethiopia. Kisha akajiunga na Muungano wa Mahakama za Kiislamu ambazo zilikuwa na mamlaka katika maeneo mengi ndani ya kusini-magharibi ya Somalia kuanzia mwaka 2006 -2007 kisha ikasambaratishwa tena na uvamizi wa Ethiopia.

Mukhtar Robow "Abu Mansur" alikuwa katika orodha ya Marekani ya Zawadi kwa Haki (RFJ) kwa mtu yeyote ambaye atasema alipo kwa kupewa Dola milioni 5 za Marekani terehe 7 Juni 2012. Kisha baadaye alitolewa katika orodha hiyo mnamo 23 Juni 2017 kutokana na mazungumzo baina ya serikali ya Amerika na serikali ya Somalia. Zaidi ya hayo ni kuwa tarehe 13 Agosti 2017 aligonga vichwa vya habari kwa kujisalimisha kwa jeshi la Somalia nakupigiwa upatu kuwa ni uamuzi/ uasi wa kihistoria. Kwa mara nyingine tarehe 4 Oktoba 2018 akagonga vichwa vya habari kwa kutangaza kuwa atagombea katika kinyang'anyiro kitakachofanyika tarehe 17 Novemba, 2018 katika Jimbo la Kusini Magharibi (SWS).

Hayo yote yanadhihirisha wazi kuwa hakika Mukhtar Robow si chochote bali ni mtumwa wa Marekani ndani ya Somalia. Kwa kuwa yeye ni maarufu na mwenye ushawishi katika koo yake, hivyo basi, kujitangaza kwake kwa uchaguzi ujao kulisukumwa na Serikali Kuu ili aweze kupambana na Sharif Hassan Sheikh Aden, ambaye wakati huo alikuwa rais wa Jimbo la Kusini Magharibi na alikuwa anazipinga sera za Mogadishu na alikuwa anagombea hatamu ya pili. Lakini mnamo 7 Novemba 2018 Sharif Hassan Sheikh Aden alijiuzulu mara moja baada ya kugundua kuwa hawezi kuhimili mchakato wa Mogadishu na umaarufu wa Robow. Kuondoka kwa Sharif Hassan Sheikh Aden ikawa ndiyo mwisho wa umuhimu wa Mukhtar Robow kwa kuwa kikwazo cha Serikali Kuu ya Somalia hakipo tena. Hivyo basi, Serikali Kuu ikahairisha uchaguzi mara tatu kuanzia 17 Novemba hadi 5 Disemba kisha 19 Disemba 2018. Zaidi ya hayo, waliishinikiza Tume ya Uchaguzi ya Jimbo la Kusini Magharibi ibatilishe ugombeaji wa Robow kwa kuwa hakupitia Mpango wa Kuwajenga Upya Waasi wa kuwatathmini waliokuwa wanachama wa Al-Shabaab. Lakini, Robow hakutaka kurudi nyuma na hivyo kuilazimisha Serikali Kuu kumtia korokoroni. Hatima yake ikiwa hakushiriki uchaguzi ambao ulishindwa na aliyekuwa Waziri wa Kawi Abdiaziz Hassan Mohamed "Laftagareen" siku ya Jumatano, 19 Disemba 2018.

Amerika inataka kuhakikisha kuwa Somalia inabakia kuwa ya kisekula kiukamilifu ikiendeshwa na vibaraka walioandaliwa kikamilifu mfano Farmaajo na wala sio watu kama "Mukhtar Robow" ambaye bado anaashiria eti Uislamu wa Misimamo Mikali lakini wanaweza kuwatumia watu aina hiyo pale watakapohisi maslahi yao yametishiwa. Licha ya malalamiko ya haki za kibinadamu kutokana na kile kinaochoitwa "zamani yao hatari" umuhimu wao unategemea maslahi ya wakoloni wamagharibi wakiongozwa na Marekani ambaye ndiye mwagaji wa damu wa kwanza ulimwenguni kote na asiyejali haki za kibinadamu kwa kuwa yeye ndiye mmiliki wa mashirika hayo. Hivyo basi, yanayomtokea Mukhtar Robow sio mageni hususan wakati huu ambapo Marekani inataka kuitia mkononi kiukamilifu Pembe ya Afrika kupitia vibaraka wake watiifu wakiongozwa na Waziri Mkuu Abiy Ahmed wa Ethiopia. Kupitia utekelezaji wa sera ya Marekani kuhusiana na Pembe ya Afrika kwa kuziunganisha Ethiopia, Eritrea, Somalia na Djibouti. Hivyo basi, Amerika imemteua Donald Yamamoto kama Balozi wa Somalia baada ya takribani miaka 28 tokea kuangushwa kwa utawala wa kibaraka wao Siad Barre 1991.


Utawala wa Somalia lazima uamke na ufahamu kwamba ushindi, hadhi na cheo cha kweli vinatokamana na amani, usalama na utulivu wa kweli ambao utapatikana tu kwa kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu (swt). Nayo ni kwa wao kujisalimisha kwa utawala wa Mwenyezi Mungu (swt) kupitia kukumbatia ulinganizi wa kurudisha tena maisha ya Kiislamu kwa kusimamisha Khilafah. Khilafah itakayo tawala/hukumu kwa Qur'an na Sunnah na sio kwa mfumo wa kisekula wa kirasilimali na nidhamu zake zinazonuka na ikijumuisha ile inayoitwa utawala wa nidhamu ya kidemokrasia, ambayo inadaiwa kuwa ndiyo muongozo sio tu wa Somalia bali wa ulimwengu wote.

وَمَنْ أَحْسَنُ مِنَ اللهِ حُكْماً

"Na nani aliye mbora zaidi katika Kuhukumu kuliko Mwenyezi Mungu"

**Ali Nassoro Ali**

**Mwanachama wa Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Kenya**



# Njia ya Mtume (saw) Kuleta Mageuzi

## Halaqa 20: Hatua ya Kuchukua Uongozi kwa Ummah

Ili kutabikisha (kuutawalisha/kutekeleza) Uislamu kamili na kufanya hukumu ni ya Mwenyezi Mungu pekee. Katika Halaqa hii tutazungumzia hatua (marhala) ya tatu katika hatua za Da'awah ya Mtume (saw), nayo ni kuchukua uongozi na kusimamisha dola/serikali.

**Nukta ya Kukita**

Tunamaanisha mahali au sehemu ambayo itakuwa na mujtama mzuri ili kusimame dola na kwamba watu wa mji wabebe fikra za Uislamu, na watoe Nusra wote. Ama kundi lenye nguvu lipeane Nusra ili Uislamu ufike katika uongozi, kwani uungwaji mkono na watu jumla unaotokana na rai jumla (aam), inayochimbuka kutokana na utambuzi jumla (waa'yi aam), kipekee haifikishi Uislamu katika utawala, bali nguvu za kimada zinazo andaliwa na wenyeji kujitolea kufa kupona katika Njia ya Mwenyezi Mungu ili apewe utawala Mtume (saw) ndio inayoweza – baada ya tawfiq ya Mwenyezi Mungu- kufikisha Uislamu katika uongozi.

Hatua ya tatu imeanza kwa kusimama dola ya Kiislamu katika mji wa Madina Munawara baada ya kupita Bay'ah ya Aqaba ya pili, na zikaanza kuteremka aya, na wakapata wepesi Waislamu wakati huo kupigana Jihad na maadui zao kwa nguvu zao.

Na hapa hatuna budi kusimama katika bay'ah ya pili, kwani katika msimu wa Hijja mwaka wa 13 kutoka kutumilizwa Mtume (saw), Maanswari walimpa bay'ah (kiapo cha utiifu) Mtume (saw) Bay'ah ya Aqaba ya pili.

Hii Bay'ah (kiapo cha utiifu) sio Bay'ah juu ya utume, bali ni Bay'ah ya uongozi na utawala, ni Bay'ah ya utendajikazi, sio Bay'ah ya kusadikisha, alipewa Bay'ah Mtume (saw) kama kiongozi/mtawala na si kwa utume na unabii, kwa sababu kukubali utume na unabii ni imani, na hailazimishi kufanywe Bay'ah, kwa hiyo kumfanyia Bay'ah Mtume (saw) ni kwa kumchukulia kama raisi wa serikali, walimpa Bay'ah ya vita, kumpiga vita mwekundu na mweusi, walimpa Bay'ah ili wamhami na wamhifadhi kwa kile wanachohifadhi nacho wake zao na watoto wao... Walimpa Bay'ah ya kusimamisha serikali ya Kiislamu, ambayo atakua Mtume (saw) ndiye mtawala na raisi wa serikali, anaamrisha akitiiwa na amri yake inatekelezwa katika kila hali.

IKATIMIA HIJRA, NA SERIKALI IKASIMAMISHWA, SILAHA IKABEBWA, NA MIVUTANO YA DAIMA IKAANZA KATI YA DOLA YA KIISLAMU NA DOLA ZA KIKAFIRI.

Na ilikuwa miaka michache tu ikaweza kumalizwa dola ya kishirikina na ukafiri, likasafishwa Bara Arabu, ikatanda Njia ya Mwenyezi Mungu, na Uislamu ukabebwa nje ya bara hilo kwa DA'WAH na JIHAD.

Maanswar walitekeleza Bay'ah yao (kiapo cha utiifu) kwa Mtume (saw) mpaka akaimba muimbaji wao kwa furaha ya Tukio hili:

**Sisi Ndio tuliompa Bay'ah Muhammad**
**Juu ya Jihadi kwa umri wetu milele**

# SWALI/JAWABU:
# Makubaliano ya Sweden na Athari Yake Juu ya Janga la Yemen

**Swali:**

Mnamo 18/12/2018, tovuti ya kituo cha runinga ya France 24 iliripoti: "Ghasia zilizuka katika mji wa Hodeidah nchini Yemen kati ya majeshi tiifu kwa serikali na Mahouthi, dakika chache baada ya makubaliano ya kusitisha vita yaliyofungishwa na Umoja wa Mataifa kukamilika…" (France 24, 18/12/2018). Mnamo 17/12/2018 tovuti ya Arabic.Sputniknews iliripoti: "Mwanachama wa ujumbe wa Ansar Allah alisema kuwa makubaliano ya Sweden hayakujumuisha kuisalimisha bandari ya Hodeidah au kuondoka kwa Mahouthi kutoka mjini humo, ambapo Waziri wa Habari wa Yemen Muammar al-Iryani alijibu kwa kusema kuwa taarifa hizi zinafahamika kama mapinduzi dhidi ya makubaliano yenyewe, ambayo wino wa saini yake bado haujakauka (ungali majimaji), akisisitiza kuwa makubaliano hayo yalitaja kujiondoa kwa wanamgambo hao kutoka Hodeidah na bandari zake, Hodeidah, Salif na Ras Issa." Swali ni: ni vipi kuna sintofahamu katika maandishi ya makubaliano hayo wakati wino wa saini yake ungali majimaji?! Na ni vipi ghasia zizuke dakika chache tu baada ya kutekelezwa kwake? Kwa hiyo ni kwa nini Amerika na Uingereza zinayakaribisha makubaliano hayo? Je, janga hilo la Yemen linatarajiwa kumalizika kwa makubaliano haya? Allah akujazi kheri.

**Jibu:** Kabla ya kwenda katika kadhia ya Makubaliano ya Yemen, ambayo mazungumzo yake yalianza mnamo Alhamisi 6/12/2018 na kumalizika kwa kupeana mikono wazi mnamo 13/12/2018, hali ya Yemen inapaswa kufupishwa kama ifuatavyo:

**Kwanza,** baada ya Mahouthi kuchukua udhibiti wa Sanaa na baada ya kufurushwa kikweli kwa serikali ya Hadi kutoka katika mji mkuu huo, na kuchukua udhibiti wa maeneo mengi ya Yemen, walikuwa na haja kubwa ya kuwa na baadhi ya "uhalali" katika utawala wao. Amerika ilijaribu kuwatafutia "uhalali". Lakini hili halikuwa rahisi, kwa kuwa kitovu cha kisiasa cha Yemen kwa kiasi kikubwa kinaegemea kwa Uingereza, kwa hivyo matarajio makubwa kabisa ya Amerika yalikuwa ni kukubali kwa Mahouthi kuwa kama sehemu muhimu ya ramani ya kisiasa ya Yemen. Mahouthi ni wachache eneo la Kaskazini mwa Yemen hususan mjini Saada, na hawakubaliki miongoni mwa watu jumla, kwa hivyo Amerika ilifanya kazi kuwasaidia Mahouthi hawa ili wawe watu muhimu nchini Yemen ili kusiendelee utawala wowote pasi na wao, na hili ni kupitia hatua zifuatazo:

1- Iliifanya Saudi Arabia kushambulia kupitia operesheni ya angani "dhoruba kali", sio kuwamaliza Mahouthi; vyenginevyo, wangepeleka majeshi ya nchi kavu, lakini ili kuwaonyesha Mahouthi kama watetezi wa Yemen mbele ya ndege za kivita, wakionekana kama waliodhulumiwa na wakati huo huo kama mashujaa, na hivyo basi kupata umaarufu wa kukubaliwa na rai jumla.

2- Hadi, Raisi wa Yemen mtiifu kwa Waingereza, alifanywa kama mateka nchini Saudi Arabia, na hivyo wanaweza kumtia shinikizo kwa urahisi kila mipango hiyo inapohitaji.

3- Ililishawishi Baraza la Usalama kutuma wajumbe nchini Yemen walio na utiifu kwa Amerika, na kufaulu katika hili, hivyo basi, Jamal bin Omar, na Ould Cheikh walitumwa.

Uingereza, ambayo imekuwa na ushawishi nchini Yemen kwa miongo kadhaa, inajua kuwa harakati ya eneo la kusini na Mahouthi eneo la kaskazini ni vyombo vya Amerika vya kupenyeza ushawishi wake mkubwa nchini Yemen. Kupitia kuingia kwa Mahouthi jijini Sanaa na kwengineko nchini Yemen na kufaulu kwao kupata usaidizi mkubwa wa kijeshi wa Iran, Uingereza iliona kuwa ushawishi wake nchini Yemen umeanza kuyumba, hususan baada ya dori ya Saudia nchini Yemen, hivyo basi Uingereza ilikimbilia kujibu mipango na ala za Amerika:

a- Dori iliyochezwa na Imarati sambamba na ile dori ya Saudia. Hakika, Imarati ilicheza dori muhimu sana katika kurudisha mji wa Aden na miji mengineyo eneo la kusini kutoka mikononi mwa Mahouthi, na kupitia dori hii iliunda harakati ya eneo la kusini iliyo wapunguza makali vibaraka wa Amerika katika harakati hii na kuifanya dori yao kushika nafasi ya pili, na kuidhibiti kusini.

b- Ilimleta kibaraka wa zamani, Ali Saleh, eneo la kusini katika safu ya Mahouthi. Akawa ni mshirika wao na katika ngazi zao, ili Uingereza ishiriki katika dori na Mahouthi endapo watachukua mamlaka, na alikaribia kufaulu katika misheni yake kabla ya kumuua.

c- Ilifanya bidii kutuma mjumbe wa UN aliyemtiifu kwake, na iliweza kufanya hivyo, kwa hivyo Muingereza Martin Griffith aliteuliwa kama balozi mpya wa kimataifa nchini Yemen.

**Pili:** Uingereza ilijua kuwa uti wa mgongo wa Mahouthi ni usaidizi wa Iran. Baada ya kufungwa uwanja wa ndege wa Sanaa na kudhibitiwa kwa bandari za kusini, bandari ya Hodeidah ilikuwa ndio ya pekee yenye mwanya nusu wa iran wa kusaidia Mahouthi. Hii ndio sababu Imarati ilikwenda Hodeidah ili kuidhibiti. Makabiliano na vita maeneo ya Hodeidah yalikabiliwa na upinzani

*Endelea Uk..13*

mkubwa wa Amerika chini ya kisingizio cha ubinadamu, na kwamba bandari ya Hodeidah inaipa Yemen msaada kwa mamilioni ya Wayemeni kana kwamba Amerika inajali binadamu. Iliwavunja vunja vibaraka wake nchini Syria chini ya Umoja wa Mataifa kwa kuizingira miji iliyo taabani na kwa ulipuzi wa makombora.

Lakini ilitaka kutafuta uhalalishaji wa kuifanya bandari ya Hodeidah kuwa wazi kwa usaidizi wa kijeshi wa Iran, ambao kwa mwaka au zaidi ulijumuisha makombora ya angani ambayo Mahouthi walianzisha juu ya Saudi Arabia, pamoja na ndege zisizokuwa na rubani (drones) zilizo rushwa kwa kulenga maeneo makhsusi nchini Imarati. Kinyume na hayo, Saudi Arabia ilikuwa ikizungusha ndege zake pasi na mashambulizi ya kihakika ya kambi za Mahouthi, kwa mfano majeshi ya Mahouthi yaliizingira Taiz na maeneo ya vikosi vyake vya kijeshi yalianikwa kwa udhibiti wa angani na hivyo basi kambi hizo hazikuwa vigumu kuzishambulia na kuondoa mzingiro huo, ingawa mzingiro huo bado ungalipo! Kihakika Imarati ilikuwa ikipigana na Mahouthi hadi ikakaribia kuwatoa Mahouthi nje ya Hodeidah lau si kwa shinikizo la Amerika juu ya Saudi Arabia!

Hivyo basi, mipango ya Amerika na ala zake haikuafikiana na mipango ya Uingereza na ala zake. Amerika iliegemea upande wa suluhisho la kisiasa baada ya kuudhamini udhibiti wa Mahouthi juu ya sehemu muhimu za Yemen. Uingereza ilikuwa ikisubiri kushindwa zaidi kwa Mahouthi ili kukubali kujiondoa, ambako kungewafanya kurudi katika makubaliano ya Saada kabla ya kwenda katika suluhisho halisi la kisiasa. Hivyo basi, majadiliano yote ya nyuma hayakuwa chochote zaidi ya “michezo” ya kisiasa ya kupitisha wakati. Hivyo basi, mazungumzo kama hayo hayakufaulu, kama vile majadiliano ya Kuwait na majadiliano ya Geneva mwanzoni mwa Septemba, pindi ujumbe wa Mahouthi ulipo kosa hata kufika … nk. Kwa hayo, majadiliano hayo yalifeli na Mahouthi wakasimama mbele ya hatari kubwa ya kukaribia kuchukuliwa Hodeidah na bandari zake na majeshi yanayo saidiwa na Imarati, baada ya kuweko pambizoni mwake. Wakati huo huo, dori kubwa zaidi ilikuwa kwa Imarati, iliyo wapeleka na kuwasajili wanamgambo wanati kwa ajili ya vita vya Hodeidah. Saudi Arabia ilikuwa katika hali ya kufedhehesha; haikuweza kupinga mwelekeo huu wa Imarati kwa sababu ni “washirika” walio uwanjani katika vita vya Yemen dhidi ya lengo lililo tangazwa na Mahouthi! Na kwa sababu Amerika inazuia shambulizi juu ya Hodeidah, Imarati, na nyuma yake Uingereza, ilichagua muda ambapo Amerika ilijiingiza katika kadhia iliyo na shinikizo zaidi kwake. Vita vya Hodeidah vilizuka mnamo 8 na 9/6/2018 (Alhurra 10/6/2018) katika wakati ambao Amerika ilijiingiza pakubwa kwa matayarisho ya Kongamano la Trump na kiongozi wa Korea Kaskazini lililofanyika nchini Singapore mnamo 12/6/2018.

Yaani, ilichagua muda ambao Amerika takriban imepooza kutokana na kusitisha shambulizi hilo. Na ndivyo ilivyokuwa … Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa lilifeli kusitisha mapigano ya Hodeidah: “Mnamo Alhamisi Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa lilishindwa kukubaliana juu ya kukomesha mara moja mashambulizi ya Muungano wa Waarabu unao ongozwa na Saudi Arabia na Imarati juu ya mji wa Hodeidah.” (Al Jazeera Net 15/6/2018). Vita vya Hodeidah na uwezekano wa udhibiti wa Imarati na wanamgambo wanaosaidiwa nao juu ya bandari ya Hodeidah lilikuwa ndio tishio kubwa zaidi kwa utawala wa Mahouthi nchini Yemen. Hivyo basi, Mahouthi walipeleka majeshi yao yote ili kuzuia kutokea kwa haya, na Amerika ilipeleka maafisa wake kulalamikia kuhusu hali ya kibinadamu nchini Yemen na juu ya bandari ya Hodeidah kwamba ndio mwokozi wa kukomesha baa la njaa nchini Yemen. Imarati na washirika wake wa eneo walikuwa wakisubiri fursa za kimataifa ili kuanzisha mashambulizi zaidi na kujaribu kusonga mbele ardhini katika kulazimisha uhalisia uwanjani juu ya mji huo na bandari hiyo, ambao ulipatikana nusu yake na kuwa tishio kubwa kwa Mahouthi na hivyo basi kuwa ushawishi mwengine wa Amerika nchini Yemen. Katika miezi ya hivi karibuni, kuzuka kwa mapigano ya mara kwa mara maeneo ya Hodeidah imekuwa ni sehemu ya vita hatari zaidi vya Yemen. Hususan, Amerika imeshindwa kuuvuruga Muungano wa Saudia na Imarati nchini Yemen, kama ilivyo shindwa kusitisha vita katika upande wa Saudi Arabia pekee, ikiwemo uharibifu kutokana na dori ya kiuongozi ya Saudia ya dola za Ghuba, na hali ikabakia hivyo hivyo hadi ilipotokea kadhia ya fedheha kubwa sana kwa Saudi Arabia, iliyofuatiwa na kuuliwa kinyama kwa mwandishi habari wa Saudia Jamal Khashoggi mwanzoni mwa Oktoba 2018.

Tatu: kuuliwa kwa mwandishi habari wa Saudia Khashoggi jijini Istanbul kulipelekea kuibuka kwa dhurufu mpya zilizoizunguka Saudi Arabia ambazo huenda zilitumiwa kwa maslahi ya Amerika:

1- Huduma za usalama za Saudia zilitekeleza kitendo cha kinyama katika ubalozi wao jijini Istanbul, kilicho pelekea kampeni ya kimataifa dhidi ya Saudi Arabia, kisiri na wakati mwengine kidhahiri, ikitoa wito wa kuhesabiwa Mfalme Mtarajiwa wa Saudia Muhammad Bin Salman kwa kutekeleza kitendo cha kinyama dhidi ya maadili yoyote ya kibinadamu. Ingawa Saudi Arabia na watawala wengine wahalifu katika eneo la Waislamu wametekeleza maafa dhidi ya raia wake kuliko kuuliwa kwa mwandishi habari wa Saudia jijini Istanbul, lakini kitendo hiki kimezalisha hamasa za kutosha, ambazo zimepelekea shutuma kali za nchi nyingi. Nchi za Ulaya zilitaka kuzitumia ili kumdhoofisha kibaraka wa Amerika, Bin Salman, au ikiwezekana kumng’oa mamlakani, lakini Amerika ilifanya haraka kupeana sitara ya kimataifa kwa Bin Salman, kupitia tweet za Raisi Trump zilizo onyesha imani kwa kile anachosema mfalme mtarajiwa wa Saudia, hivyo basi kuondoa tuhuma hizo. Trump alisema parwanja kuwa hataachana na mikataba ya silaha na Saudi Arabia kutokana na manufaa ya kudhibiti ukosefu

Endelea Uk..14

wa ajira nchini Amerika, ambayo imeongeza shinikizo la wabunge wa Congress kwa utawala wa Trump, ambao waliutuhumu kupigia debe kile ambacho wanachama wa bunge la Congress wanakiita “maadili ya Kiamerika” kwa ajili ya pesa za Saudia. Bunge hilo la Congress kisha likatoa makemeo ya nadra ya kihistoria dhidi ya utetezi wa Raisi Donald Trump kwa Muhammad Bin Salman: (Katika makemeo ya kihistoria ya kumkemea Raisi Donald Trump, bunge la Seneti la Amerika lilipiga kura mnamo Alhamisi ili kumaliza usaidizi wa kijeshi wa Amerika kwa vita nchini Yemen na Mfalme Mtarajiwa Muhammad Bin Salman akabebeshwa masuliya kwa mauwaji ya mwandishi huyo wa habari. Jamal Khashoggi wa Saudia … katika hatua ya kihistoria bunge la Seneti lilipiga kura 56 hadi 41 ili kumaliza usaidizi wa kijeshi kwa kampeni inayo ongozwa na Saudia nchini Yemen. (Reuters, 14/12/2018)

2- Pindi wanachama wengi wa bunge la Congress walipoonyesha wasiwasi kuhusu haja ya kukomesha kuamiliana na Mfalme Mtarajiwa wa Saudia, “kibaraka mtiifu wa Amerika” na baadhi kutoa wito wa kukomesha upelekaji silaha Saudia, ambazo Trump anajingamba kwazo, kwa athari iliyo nazo katika kubuni ajira nchini Amerika, utawala wa Trump hatimaye ukakimbilia kuleta purukushani kutoka kuangazia kesi ya Khashoggi na kuituhumu Saudi Arabia kwa kadhia nyengine muhimu inayo onyesha kuwa Saudi Arabia inasimama na haki za kibinadamu, amani, na usalama, na kwamba inashirikiana na Umoja wa Mataifa. Ushirikiano wa mtoto wa Salman ulipigiwa debe wakati wa mazungumzo ya Sweden: “Afisa wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres anatarajiwa kuhudhuria mazungumzo ya mwisho nchini Sweden katika kusaidia juhudi za balozi wake wa amani nchini Yemen ili kuanza mchakato wa kisiasa kumaliza vita vinavyo endelea vya miaka minne. Shirika rasmi la Habari la Saudia lilisema kuwa Guterres alimpigia simu Mfalme Mtarajiwa Muhammad Bin Salman ili kujadili “mapya yanayo jiri katika uwanja wa Yemen, na juhudi zinazo fanywa juu yake.” (Reuters, 12/12/2018).

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres, aliangazia juu ya mchango wa Salman: Katibu Mkuu huyo wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres alifichua kwa kituo cha Al Arabiya mnamo Alhamisi dori iliyochezwa na Mfalme Mtarajiwa, Muhammad Bin Salman, katika makubaliano ya Yemen ya kihistoria leo kati ya Ansar Allah na serikali ya Yemen … Naibu Msemaji Rasmi wa UN Farhan Haq aliwaambia maripota katika makao makuu ya UN jijini New York mnamo Alhamisi kuwa Guterres alihisi kuwa mchango wa Mfalme huyo Mtarajiwa “ulikuwa muhimu mno kwa matokeo ya mashauriano hayo” (Arabic.Sputniknews 13/12/2018). Hivyo basi, Amerika iliangazia dori yake kwa njia ya kustaajabisha kufikia hadi Griffith kuwajibika kuisifu dori hii: Griffith alisema katika kongamano kwa njia ya video kutoka Jordan kuwa majadiliano kati ya pande za Yemen yalifaulu kufikia mkataba na akaongeza kusema: “Namshukuru Mfalme Mtarajiwa, Mheshimiwa Mfalme Muhammad Bin Salman, ambaye amethibitisha usaidizi wake muhimu mno wa kibinafsi kwa mchakato huu (Al-Watan News 14/12/2018) Yote haya yaonyesha kuwa Amerika inahamu ya kufanya makubaliano kwa sababu tatu:

**Kwanza:** kuimarisha sura ya Saudi Arabia, **na pili:** kuondoa fedheha ya kimataifa kutoka kwa Saudi Arabia na kuifinika kadhia ya mwanahabari wa Saudia, **na tatu:** kuitishia Saudi Arabia kifedha! Hili ni muhimu zaidi kwa Trump … kwa yakini Amerika haitaki kuimarisha sura hiyo na kuondoa fedheha machoni mwa vibaraka wake Mohammed Bin Salman na babake, lakini kwa kitendo hiki itaonekana kuwaokoa wote wawili kutokana na “balaa” na kisha kuipatiliza katika “kuifyonza” pesa zaidi kutoka katika mafuta ya Saudia kama thamani ya kuiondoa fedheha ya kimataifa kutoka kwao, na hili linaafikiana na fikra ya “upapiaji” wa kibiashara ya Trump iliyo jengwa juu ya sera ya “tulipe”!

3- Kinacho ashiria maslahi haya ya Amerika katika kufanya makubaliano hayo ni kile kinachotolewa na maafisa nchini Amerika pamoja na kutunga mamlaka ya kile kilichotolewa, ikiwemo:

“Amerika imetoa wito wa kusitisha vita nchini Yemen ndani ya siku 30, ikisisitiza haja ya kukomesha muungano wa Waarabu ukiongozwa na Saudi Arabia, kupiga mabomu maeneo ya wakaazi nchini Yemen. Waziri wa Ulinzi James Matisse alitoa wito kwa pande zote za mzozo wa Yemen kusitisha vita ndani ya siku 30, Na kuingia katika majadiliano ya umakinifu ili kumaliza vita nchini humo. Matisse alisema, wakati wa hotuba yake katika warsha iliyo andaliwa na Taasisi ya Amani ya Amerika jijini Washington, mnamo Jumanne: (“Kwa ajili ya suluhisho la muda mrefu tunataka kusitishwa kwa vita, kuondoka kutoka mpakani, na kusitishwa kwa mabomu ya angani … Pande zote husika katika mzozo nchini Yemen zinapaswa kuketi katika meza ya majadiliano katika siku 30 zijazo.” Alisisitiza kuwa “pande zinazo pigana nchini Yemen ni lazima zisonge mbele kuelekea juhudi za Amani,” aliendelea kusema kuwa: “Tunahitaji kufanya hivyo katika siku thalathini zijazo, na nadhani kuwa Saudi Arabia na Imarati ziko tayari kuendelea na jambo hilo.” (Gulf Online, 10/31/2018)

- Amerika ilimtuma Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Guterres kuhudhuria majadiliano ya Sweden na kuwatia shinikizo wajumbe wanaojadiliana ili kuhakikisha kufikia makubaliano au mwanzo wa makubaliano, na kutomuachia mambo Balozi wa Kimataifa wa Uingereza Griffith: “Katibu Mkuu wa UN Antonio Guterres anatarajiwa kuhudhuria mazungumzo ya mwisho nchini Sweden kwa usadizi wa juhudi za balozi wake wa amani nchini Yemen ili kuanza mchakato wa kisiasa kumaliza vita ambavyo vimekuwa vikiendelea kwa takriban miaka minne.” (Reuters, 12/12/2018).

- Shinikizo la Saudi Arabia juu ya Raisi Hadi wa Yemen ili

*Endelea Uk..15*

kukubali makubaliano yaliyo wasilishwa: duru ziliiambia Al-Jazeera kuwa Saudi Arabia ilimlazimisha Raisi wa Yemen Abed Rabbo Mansour Hadi ili kuongoza ujumbe wa serikali ya Yemen katika majadiliano ya Sweden ili kukubali makubaliano ya kusitisha vita katika mji wa Hodeidah na bandari zake. Duru hizo ziliripoti kuwa ujumbe wa serikali uliwasilisha waraka kwa Hadi, "anayeishi Riyadh", ukipendekeza kutotia saini makubaliano hayo kwa sababu hayaelezi wazi wazi kuwa Mahouthi wataondoka mji wa Hodeidah na bandari zake, lakini raisi wa Yemen akaelekezwa kuyatia saini baada ya shinikizo kali kutoka kwa Saudi Arabia katika masaa machache yaliyopita, kwa mujibu wa duru hiyo (Al-Jazeera.net 13/12/2018)

- Uteuzi haraka wa Jenerali wa UN ili kusimamia kusitisha vita mjini Hodeidah: "Umoja wa Mataifa, ulimchagua jenerali wa Kiholanzi, ili kuongoza misheni ya usitishaji vita baina ya pande zote za Yemen. Mjumbe wa Umoja wa Mataifa nchini Yemen, Martin Griffith, alisema jenerali huyo mstaafu wa Kiholanzi, Patrick Cammaert, alikuwa amekubali kuongoza misheni ya usimamizi nchini Yemen na kuongeza kuwa Cammaert huenda akawasili eneo hilo katika muda wa siku chache." (Yemen News, 14/12/2018). Tovuti ya maoni ya Yemen mnamo 20/12/2018 ilichapisha: "Msemaji rasmi wa UN Stephane Dujarric amesema, mwenyekiti wa kamati, jenerali mstaafu wa Kiholanzi Patrick atasafiri hadi Jordan kesho mnamo Alhamisi, kisha hadi Sanaa na kutoka huko hadi Hodeidah …"

- Amerika kuyakaribisha hadharani makubaliano hayo. Waziri wa Kigeni wa Amerika, Pompeo aliyakaribisha makubaliano hayo, akisema kuwa: "Amani inawezekana nchini Yemen" (Shirika la habari la BBC 14/12/2018). Alisema katika taarifa: "Mashauriano haya kati ya Jamhuri ya Serikali ya Yemen na Mahouthi yameashiria hatua ya kwanza muhimu … Amani inawezekana. Pande zote zina fursa ya kujenga juu ya ari hii na kuimarisha maisha ya watu wote wa Yemen na kusonga mbele, wote ni lazima waendelee kuwasiliana, kuzima taharuki, na kusitisha uhasama unaoendelea." (Yemeni Scene, 14/12/2018)

- Mawasiliano thabiti ya Balozi wa Amerika na Mahouthi: "Balozi wa Amerika nchini Yemen, Matthew Toller, alisema wakati wa uhudhuriaji wake katika kongamano na majadiliano jijini Stockholm: "Tulifanya mkutano rasmi baina ya mabalozi na kundi, akiwemo mwanachama wa ujumbe wa Houthi … Kivyangu nilikuwa na mawasiliano na baadhi ya watu katika timu ya Mahouthi katika sehemu walioisifu kuwa nzuri, hakika ni mkutano mzuri." Aliulizwa kama mkutano huo pamoja nao ulikuwa wa moja kwa moja na rasmi, alisema: "Mkutano wowote ninaofanya ni rasmi, Mimi ndiye balozi wa Amerika nchini Yemen masaa 24 kwa siku" (Saudi Arabia, Middle East, Arab News 13/12/2018).

**Nne:** Ingawa makubaliano hayo ya Sweden yalikuwa chini ya shinikizo la Amerika na kisha kuyakaribisha kama tulivyosema juu, Uingereza vilevile iliyakaribisha kwa sababu Amerika ilijenga rai jumla yenye shinikizo kubwa kuhusu malengo ya kibinadamu na majanga ya baa la njaa nchini Yemen na maradhi ya watoto kutokana na vita na wafu na majeruhi nk…, kana kwamba mambo haya yamezuka leo! Hivyo basi, mazingira yaliyo jengwa na Amerika ili kutamatisha makubaliano hayo hayakuacha khiari kwa Uingereza isipokuwa kuyakaribisha, lakini kwa njia yake ya kusukuma wimbi la kubadilisha kituo chake au angaa kupunguza kasi yake, iliyakaribisha makubaliano hayo: Wizara ya Kigeni ya Uingereza mnamo Jumanne, ilikaribisha usitishaji vita nchini Yemen … Waziri wa Kigeni wa Uingereza Jeremy Hunt alisifu juhudi za Mjumbe Maalumu wa Umoja wa Mataifa nchini Yemen, Martin Griffith, katika nukuu ya tweet katika mtandao wa Twitter wa Afisi ya Kigeni ya Uingereza … (Chanzo: Yemen Net 18/12/2018)

Wakati huo huo ilisalimisha azimio kielelezo kwa Baraza la Usalama ili kujadili makubaliano hayo kwa kisingizio cha namna ya kuyatekeleza:

"Uingereza inatafuta azimio jengine la Baraza la Usalama la UN na kuwasilisha azimio kielelezo kwa Baraza hilo kwa ajili ya mazungumzo," Mjumbe wa Uingereza katika UN Karen Pierce alisema: "Kama mshikiliaji faili ya Yemen katika Baraza hilo la UN, Uingereza itaregelea kufanya kazi na wandani wote katika azimio la Baraza la Usalama ili kuidhinisha makubaliano hayo yaliyofikiwa na pande zote, kusaidia utekelezwaji wake na kuwezesha Umoja wa Mataifa kusimamia utekelezaji kwa pande zote na kuweka hatua nyengine za haraka." (Tovuti ya Vijana wa Yemen ikinukuu tovuti ya serikali ya Uingereza, 14/12/2018).

- Mnamo Jumanne, mabalozi walisema: Baraza la Usalama la UN inalichunguza azimio kielelezo la Uingereza linalomtaka Katibu Mkuu wa UN Antonio Guterres kusalimisha mapendekezo kufikia mwishoni mwa mwezi huu juu ya namna ya kusimamia usitishaji vita mjini Hodeidah, na Uingereza imesambaza azimio hilo kielelezo ili kuunga mkono makubaliano hayo katika Baraza la Usalama. Haijulikani lini litapigiwa kura, ambapo azimio hilo lahitaji kura 9 kulipitisha na hakuna matumizi ya haki ya kura ya turufu kwa Amerika wala Ufaransa wala Uingereza wala China wala Urusi … (Al-Ain News, 18/12/2018)

Uingereza iliwasilisha mradi huu kama udhuru wake ili kuhusishwa katika makubaliano hayo kwa kisingizio cha namna ya kudhibiti na kutekeleza na kujiondoa, kurefusha, ili pande zinazo zozana katika biladi ya Yemen zisiwe na wasiwasi kuhusu idadi ya wanaofariki katika watu wake na kiwango cha uharibifu katika majengo yake bali maslahi yao yapatikane. Hivyo basi, twaweza kusema:

Amerika na washirika wake katika eneo hilo, hususan

Endelea Uk..16

Saudi Arabia, wako makini kuhusu kumaliza vita vya Yemen leo na kuongoza majadiliano yanayopelekea kupata hisa kubwa ya utawala wa Yemen kwa Mahouthi, wafuasi wa Iran na hivyo basi wafuasi wa Amerika. Umakinifu wa hili ulionekana kupitia kufanya majadiliano ya Sweden. Lakini mwelekeo huu wa Amerika haumaanishi kuwa Amerika yaweza kuupata chini ya ushawishi wa Uingereza nchini Yemen. Uingereza ilimtuma Waziri wake wa Kigeni kwenye majadiliano ya Sweden mnamo 13/12/2018 ili kumsaidia mjumbe wake wa kimataifa Griffith mbele ya Raisi wake Guterch, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa; hii ndio sababu makubaliano hayo yalifungika kwa Hodeidah pekee, na faili nyenginezo, hususan uwanja wa ndege wa Sanaa, ziliakhirishwa kwa raundi za mbeleni. Vile vile misimamo ya ujumbe wa serikali ilikuwa na shauku ya utekelezwaji wa yale yalioafikiwa, ikiashiria kuwa ilikuwa chini ya shinikizo la Saudi Arabia na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, na Amerika nyuma yao.

Al-Yamani alisema wakati wa mkutano wa waandishi habari uliofanywa katika tamati ya majadiliano katika mji wa Sweden wa Rimbo kuwa serikali ya Yemen ilikamilisha makubaliano 75 pamoja na Mahouthi, lakini hawakujifunga nayo. Aliwatuhumu Mahouthi kukataa kuondoa mzingiro wao wa mji wa Taiz … Kuhusiana na faili ya uwanja wa ndege wa Sanaa, al-Yamani alisema kuwa serikali ilikuwa tayari kuufungua kwa safari za ndege za kimataifa kupitia uwanja wa ndege wa Aden, lakini Mahouthi wakakataa mpango huu. Al-Yamani alisema kuwa "mradi wa kumaliza mapinduzi haya unaanza na Hodeidah." Alisema Umoja wa Mataifa na jumuia ya kimataifa zinabeba masuliya ya kuwalazimisha Mahouthi kutekeleza makubaliano hayo juu ya Hodeidah na ubadilishanaji wa wafungwa … Akichangia tangazo la Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres la mipango ya kufanya raundi mpya, alisema: "Raundi mpya za mashauriano hazipaswi kufikiriwa isipokuwa hii ya sasa iliyo afikiwa itekelezwe." (Russia Today, 13/12/2018). Yote haya yanafungua mlango wa kukiuka pakubwa makubaliano haya wakati wa utekelezaji wake na kuchelewesha kufanya raundi nyenginezo.

Hivyo basi, inatarajiwa kuwa utekelezaji wa makubaliano ya Hodeidah utakuwa mgumu, kama ilivyo ashiriwa na ghasia zilizotokea mnamo 14 na 15 na 16/12/2018 pambizoni mwa mji wa Hodeidah, muda mfupi baada ya tangazo la makubaliano ya Sweden, ambapo Umoja wa Mataifa ulilazimika kuyahalalisha: duru ya UN ilisema: "Huku Makubaliano ya Hodeidah yakieleza kusitishwa kwa vita mara moja, ni kawaida kwa kadhia kuchukua masaa 48 au 72 kwa maagizo kutekelezwa uwanjani … Tunatarajia kuwa usitishaji vita hivyo utabikishwa kuanzia Jumanne." (Reuters, 16/12/2018)

Hivyo basi, inatarajiwa kwa hali kwenda mbele na nyumba. Kwa upande mmoja, Amerika inataka kufunga mandhari ya kijeshi, hususan mjini Hodeidah na bandari zake, na kisha kuendelea na suluhisho za kisiasa pamoja na kudumu kwa "sauti" ya Mahouthi yaani Hodeidah. Kwa upande wa Uingereza, kuna visingizio vya kuendelea na vita ili kufikia kwa kadri iwezekano kuwadhoofisha Mahouthi na kuwanyamazisha mjini Hodeidah kabla ya kuelekea katika suluhisho la kisiasa.

**Tano:** Ama kuhusu swali la mwisho (na je inatarajiwa kuwa makubaliano haya yatamaliza mgogoro wa Yemen?) Ni kama ifuatavyo:

Makubaliano haya hayatatui mgogoro huu nchini Yemen kutokana na mgongano wa maslahi ya Amerika na Uingereza na ala zao za kieneo walioyatia saini. Matokeo yake makubwa ni kuleta tu baadhi ya utulivu kama mapumziko kwa mpiganaji na kisha mambo yatachemka tena, na huenda kwa njia ya warasilimali yakajumuisha maridhiano kama kanuni inayo shirikianwa na pande zote mbili kwa mujibu wa mizani ya nguvu za pande zote mbili. Na bila shaka, hili halimalizi mgogoro huo; yaani, matukio nchini Yemen yataendelea kupanda na kushuka, kupoa, na kisha kuwaka tena kwa mujibu wa mizani ya nguvu za kisiasa na kijeshi katika mzozo huo. Kitakacho umaliza ni moja ya mambo mawili kama ilivyo tajwa katika matoleo yaliyo tangulia:

**Kwanza** ni kuwa Amerika au Uingereza yaweza kutatua mambo kwa manufaa yake na kutawala ushawishi nchini Yemen. Hili liko mbali na kupatikana, kama ambavyo tayari tushafafanua.

**Pili** liko karibu kwa idhini ya Allah kuwa Allah ataukirimu Umma huu kwa Khilafah, ili ushawishi wa makafiri na wakoloni hawa ung'olewe kutoka katika biladi hii na maovu yao yaondolewe miongoni mwa watu. Na ili ukafiri na watu wake wafedheheshwe na Uislamu na Waislamu wafate izza na waumini wafurahie ushindi wa Allah

وَيَوْمَئِذٍ يَفْرَحُ الْمُؤْمِنُونَ بِنَصْرِ اللَّهِ يَنْصُرُ مَنْ يَشَاءُ وَهُوَ الْعَزِيزُ الرَّحِيمُ

"Na siku hiyo waumini watafurahi kwa nusra ya Allah. Humnusuru Amtakaye na Yeye ndiye Mwenye nguvu, Mwingi wa rehma" [Ar-Rum: 4-5]

Na watu wa Yemen, watu wa Iman na hekima, ni lazima watathmini jambo hili ili washinde duniani na akhera, na Allah ndiye msaidizi wa watu wema.

**13 Rabii' al-Al-Akhar 1440 H**
**20/12/2018 M**